



Adhabu


- ✍ Adelheid Marie Bwire
- 👥 Melany Pietersen
- 💬 Monica Shank Lauwo, Lauwo George
- 🗣 Kiswahili
- 📊 Level 2



Siku moja, mama alileta matunda mengi.



“Tutakula matunda lini?” tunauliza.
“Tutakula matunda leo jioni,”
mama anasema.



Kaka yangu Rahim ni mlahi.
Anaonja onja matunda yote.
Anakula matunda mengi.




“Angalia Rahim alichokifanya!”
mdogo wangu analalamika kwa
sauti. “Rahim ni mtundu na
mchoyo,” ninasema.



Mama amekasirishwa na Rahim.



Sisi pia tumekasirishwa na Rahim.
Lakini Rahim haombi msamaha.



“Hutamwadhibu Rahim?” mdogo wangu anauliza.



“Rahim, muda si mrefu utajuta,”
mama anaonya.



Rahim anaanza kuhisi kuumwa.



“Tumbo langu linauma sana,”
Rahim ananong’ona.



Mama alijua hili litatokea. Matunda yanamwadhibu Rahim!



Baadaye, Rahim anatuomba msamaha. “Kamwe sitakuwa mlafi tena,” anaahidi. Na sote tunamwamini.



Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Adhabu

Written by: Adelheid Marie Bwire

Illustrated by: Melany Pietersen

Translated by: Monica Shank Lauwo, Lauwo George

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](http://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).